

Kwanini Watu Wema Wanateseka?

Labda wewe ni miongoni mwa watu ambao wanajitahidi sana kufanya yaliyo mema machoni pa Mungu na kusaidia jamii. Hata hivyo pale unapopata mateso maishani labda kwanini ninateseka hata ingawa nimejitahidi kufanya yote yaliyomema! Endapo umefikia hatua hiyo na kujiuliza maswali hayo, nakutia moyo kuwa hauko pekeyako. Na kwakweli kwa silika ya mwanadamu ya kupenda haki, kuona wanadamu wema wanateseka ni lazima kutatokea maswali kama hayo na hata zaidi labda ukatilia shaka kusudi la Mungu kutuumba au hata kuwepo kwake.

Lakini hebu tulia kidogo na utafakali visababishi vyote vya kuteseka. Hapa chini nimeorodhesha baadhi, ona kama ni vyote:

- 1.) Kuteseka kwingi kwa mwanadamu kunatokana na kurithi dhambi ya asili kutoka Adam na Hawa.

- 1.1)Kwanza kabisa dhambi ni nini?:** - kwa kawaida tunaitafsiri dhambi kama matendo mabaya ambayo mtu anafanya. Hata hivyo Biblia inafafanua dhambi kuwa ni hali ya kukosa utukufu/utakatifu wa Mungu ambayo binadamu wote – wazuri na wabaya tumeirithi kutoka kwa Adam na Hawa.

Romans 5:12 *“kupitia Adam dhambi iliingia Ulimwenguni” na sehemu ya pili ya mstari huo inasema “Hivyo uzao wote wa Adam ukahesabiwa kuwa wenye dhambi” Matokeo ya dhambi yanaelezwa katika Romans 3:23 ni kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Dhana hii ya kwanini dhambi ilipitishwa kwa Watoto wa Adam na mpaka sasa hivi ni sawa kabisa na ukweli kuwa vinasaba vya wazazi vyenye magonjwa ya kurithisha vinapitishwa kwa Watoto; Wazazi wenye saratani kupitisha vinasaba hivyo kwa mtoto. Au umepata kujiuliza endapo Wazazi wote wakiwa Alibino inawezekana kupata mtoto wa kawaida? Lakini endapo mzazi mmoja ni Albino na mwingine ni wakawaida, upo uwezekano wa baadhi ya Watoto kutokuwa Albino (lakini Adam na Hawa tunaweza sema wote walikuwa Albino) Katika Ayubu 14:4 tunasoma “Ni nani anayeweza kutokeza mtu safi kutokana na mtu asiye safi? Hakuna awezaye!”*

- 1.2)Kupungukiwa huku na Utukufu wa Mungu ndiyo kunatusababishia hitilafu za kimwili kiakili na vile vile kuwa na mielekeo mibaya ya kuwaumiza watu wengine:-**

- Unakuta mtu anajua kabisa madhara ya mienendo Fulani ya Maisha, au kitu falani mfano kuvuta sigara, kutimia madawa ya kulevya au uasherati lakini bado anafanya maamuzi yasiyo na busara. Romans 7:21 inasema *“Ninapotaka kufanya yaliyo sawa, yaliyo mabaya yapo pamoja nami”*
- Aidha sisi wote tunaathiriwa na maamuzi yetu yasiyo na busara; kitu ammbacho Mungu hawezi fanya. Galatians 6:7 inasema *“Iolote analopanda mtu, ndilo atakalovuna pia”*
- Wanadamu tuna mielekeo mibaya ya kuwaumiza wanadamu wengine nah ii iko sana kwa wanadamu wenye Mamlaka hasa kutokana na Ubinafsi na pupa. Muhubiri 8:9 inasema *“...mwanadamu amemtawala mwanadamu mwenzake kwa kumuumiza”*

- 2.) Visababishi vingine vya kuteseka vinatokana na wakati na matukio yasiyotarajiwa. Hii inahusishwa na majanga ya asili, vita na uzee. Muhubiri 9:11 says *“wakati na matukio yasiyotarajiwa huwapata wote.”*

Je kuteseka kutakuja kwisha, au kufikia mwisho siku moja?

Kwanza kabisa tunapaswa kujua kuwa kuteseka haimaanishi kwamba Mngu anatuadhibu! Badala yake kuteseka huku ni makosa yetu sisi wenyewe wanadamu Kuanzia Babu na Bibi yet una hata sasa hivi kutokana na mtindo wa Maisha yetu. Hata mjanga yanayotokana na mashambulizi ya Wanyama, majanga ya asili yote haya yalianza kutathiri baada ya mwanadamu kumuasi Mungu. In English we say after Adam sinned, he also lost the harmony he had between him and God's creation (yaani alipoteza upatano wake na uumbaji wa Mungu). Romans 8:22 inasema "Kwa maana tunajua kwamba uumbaji wote unaendelea kuugua pamoja na kuwa katika maumivu pamoja mpaka sasa".

Hivyo kwa wakati uliopo mpaka hapo Mungu atakapoingilia kati kukomesha kuteseka kila mmoja wetu inabidi ajitahidi kushikilia na kutenda kulingana na viwangi vya Mungu vinavyopatikana kwenye Biblia ili kupunguza athari za mielekeo yetu ya dhambi ambayo inatusababishia kuteseka. Isaiah 48:17&18 say *"Mimi, ni Mungu wako,*

Ninayekufundisha ili ujifaidi mwenyewe,Ninayekuongoza katika njia unayopaswa kutembea.. Laiti ungesikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingekuwa kama mto."

Kama suluhisho la milele Mungu anaahidi katika Ufunuo 21: 3& 4 Naye atafuta kila chozi kutoka katika macho yao,na kifo hakitakuwapo tena,wala maombolezo wala kilio wala maumivu hayatakuwapo tena. Mambo ya zamani yamepitilia mbali."

Mungu atatimiza yote haya kupitia Ufalme wake ambao Biblia inautambulisha kuwa ni SERIKALI KAMILI kama unavyoona serikali za nchi mbalimbali duniani leo. Lakini utofauti wake ni kuwa RAIS (MFALME) wa seriali ya Mungu nu YESU ambaye yeye hana ubinafsi, hana ufisadi wala upendeleo. Serikali hii ikisimama inamaana itaziondoa serikali zote nyingine. —**DANIEL 2:44**. Cha kufurahisha mwaka 2029 ambao unakaribia kwa haraka sana utakuwa ni mwaka wa 2000 tangu YESU alipotambulishwa rasmi kama Mesiha!!